



Mfumo wa Ubora wa Taifa

Maana ya NQF kwa wewe

Mfumo wa Ubora wa Taifa (NQF) kwa Elimu na Utunzaji wa Utoto Mapema unasaidia kuhakikisha mtoto wako atapewa mwanzo mzuri zaidi uwezekanao katika maisha yake.

NQF ina viwango vya ubora kuboresha elimu na utunzaji kwa utunzaji wa siku nzima, mashule ya chekechea, mashule ya awali na huduma za utunzaji nje wa masaa ya shule.

Faida kwa familia

- utunzaji na uangalifu zaidi wa binafsi kwa watoto
- msaada mzuri zaidi kwa kujifunza na maendeleo ya watoto
- walimu wenye ustadi zaidi na sifa
- uwiano mzuri zaidi wa mwalimu kwa mtoto katika huduma mengi zaidi
- mfumo mpya wa kukadiria ubora wa huduma za elimu na za utunzaji.

Mfumo mpya wa kukadiria ubora

Kiwango cha Ubora wa Taifa ni sehemu ya NQF. Kinaweka alama teule ya juu zaidi kwa huduma zote za elimu na za utunzaji wa watoto wa Australia.

Huduma yako itapewa kadirio kwa kila eneo la maeneo hayo saba ya ubora, na kadirio la jumla.

1 Mpango na matendo ya elimu

2 Afya na usalama wa watoto

3 Mazingira ya kimwili

4 Mipango ya wafanyakazi

5 Mahusiano na watoto

6 Ushirikiano na familia na jumuiya

7 Usimamiaji wa uongozi na huduma

Makadirio ya Kiwango cha Ubora wa Taifa

Huduma ya mtoto wako itawezekana zaidi kupokea mmojawapo ya makadirio matatu ya kati chini.

Mfumo wa makadirio umepangwa ili familia na walimu wanafahamu elimu na utunzaji wa ubora ni nini, na kwamba ubora utazidi na kuendelea – hii ni kuendelea kuboresha.

Unaweza kuahidiwa kwamba huduma zinaangalia sana afya na usalama. Usalama na afya ya mtoto wako ni muhimu siku mzima, kila siku.

Maendeleo Mengi Yanahitajika

Huduma haifikii mmojawapo wa maeneo saba ya ubora au sehemu ya sheria na kuna hatari isiyokubaliwa kwa usalama, afya na ustawi wa watoto.

Tendo la mara moja litafanywa kutatua maswala.

Kuwa karibu Kufika Kiwango cha Ubora wa Taifa

Huduma inaweza kufika Kiwango cha Ubora wa Taifa katika anuwai ya maeneo, lakini kuna eneo moja au maeneo zaidi limetambuliwa kuhitaji kuboresha.

Kufika Kiwango cha Ubora wa Taifa

Huduma inafika Kiwango cha Ubora wa Taifa. Huduma inatoa elimu na utunzaji wa ubora katika maeneo yote saba ya ubora.

Kupita Kiwango cha Ubora wa Taifa

Huduma inapita mahitaji ya Kiwango cha Ubora wa Taifa katika angalau manne ya maeneo saba ya ubora.

Bora sana

Huduma inasaidia kusimamia elimu na utunzaji wa pekee, kuonyesha uongozi wa sekta, na kuahidi kuendelea kuboresha.

Kadirio linaweza kuzawadia na ACECQA tu.

Huduma zinazokadiriwa na Kupita Kiwango cha Ubora wa Taifa zinaweza kuchagua kuomba kwa kadirio hilo.

Kujifunza zaidi kuhusu NQF na jinsi inavyokuathiri na mtoto wako, ongea na huduma yako au tembelea tovuti ya Mamlaka ya Ubora wa Elimu na Utunzaji wa Watoto wa Australia (ACECQA):

www.acecqa.gov.au/families